

## **Kuzuia Virusi vya Korona (COVID-19):**

### **Masharti ya Jumla ya Mahali pa Kazi – MUHTASARI**

*Department of Labor & Industries (L&I) inawataka waajiri kuweka mazingira ya kazi salama na ya afya na kutekeleza amri ya Gavana ili kuzuia kuenea kwa virusi vya korona.*

### **Masharti ya Jumla ya Lazima kwa Waajiri**

#### **Umbali wa Mtu na Mtu**

- Hakikisha wafanyakazi wanakaa angalau miguu sita kutoka kwa wafanyakazi wenzao na umma kadri inavyowezekana.
- Ikiwa umbali wa mtu na mtu haiwezekani, tumia vizuizi na njia ningine ya kujikinga zilizoidhinishwa ili kuzuia maambukizi ya virusi vya korona.
- Hakikisha matumizi ya vikinga uso vya nguo, barakoa, au vifaa vya kupumulia pale umbali wa mtu na mtu unaposhindimana.

#### **Kunawa Mikono Mara kwa Mara na kwa Usahihi**

- Toa vifaa vya kudumu au vinavyobebeka vyenye maji safi na ya moto au ya vuguvugu, sabuni, na taulo la karatasi.
- Weka sharti la kunawa mikono unapofika kazini, unapopumzika, unapoenda bafuni, au kabla na baada ya kula, kunywa au kutumia bidhaa za tumbaku, na baada ya kugusa sehemu yenye maambukizi.
- Weka sehemu/vifaa vya kuulia vimelea, safisha au futa klwenye chombo kinachobebeka ili kuwezesha kuua vimelea mikono mara kwa mara (katikati ya kunawa mikono) baada ya kushika vitu vinavyogushwa na wengine.

#### **Usafishaji na Uuaji Vimelea wa Mara kwa Mara au wa Ziada**

- Panga ratiba ya utunzaji wa nyumba ambayo inajumuisha usafishaji na uuaji wa vimelea wa mara kwa mara.
- Hakikisha kuweka vifaa vya kutosha vya usafi mkubwa na uuaji wa vimelea baada ya kushukiwa kwa maambukizi ya COVID-19.
- Ua vimelea katika sehemu inayoguswa sana mara kwa mara.
- Hakikisha wafanyakazi wanatumia glavu za kujikinga na vikinga macho/uso wanaposhughulikia kemikali.
- Hakikisha magari ya kazini yanayotumiwa na watu wengi yanasa fishwa na kuuliwa vimelea kila mara wafanyakazi tofauti wanapolitumia gari na mara kwa mara kama watu walewale wanalitum,ia.
- Weka Karatasi za Data za Usalama (SDSs) kwa viua vimelea vyote kwenye sehemu ya kazi.

#### **Weka Kwa Wafanyakazi Wagonjwa**

- Weka masharti kwa wagonjwa kubaki nyumbani au waendelee kujitenga ikiwa wapo kwenye makazi ya shamba.
- Watambue na uwarudishe nyumbani wafanyakazi wanaoonyesha dalili za homa ya COVID-19.
- Weka uzio kwa muda mareo hayo hadi yatakapofanyiwa usafi mkubwa na kuuliwa vimelea baada ya taarifa ya mfanyakazi kushukiwa au kuthibitika kwa na homa ya COVID-19.

#### **Elimu kwa Mfanyakazi kuhusu Hatari za COVID-19 Mahali pa Kazi**

Kwa Igha inayoleweka vema na wafanyakazi, hakikisha wanafahamu:

- Viashiria, dalili, na vitu vya hatari vinavyohusiana na homa ya COVID-19.
- Jinsi ya kuzuia kuenea kwa virusi vya korona kazini.

- Jinsi ya kunawa mikono na sabuni na maji kwa angalau sekunde 20.
- Umuhimu wa kuziba kikohozi na chafya, na kutogusa uso na mikono isiyosafishwa.

\* Huu ni muhtasari. Kwa taarifa zaidi, angalia F414-164-000 *Coronavirus (COVID-19) Prevention: General Requirements and Prevention Ideas for Workplaces*.